



CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI DODOMA – TANZANIA

S.L.P. 138
DODOMA
Tanzania

Simu: +255 26 2963037
Nukushi: +255 26 2963036
Barua pepe: rector@irdp.ac.tz
Tovuti: www.irdp.ac.tz

MAELEKEZO YA UDAHILI WA KOZI ZA ASTASHAHADA (CERTIFICATE) KWA MWAKA WA MASOMO 2022/2023.

Mkuu wa Chuo Cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) anawapongeza wahitimu wote wa kidato cha nne. Kwa wanafunzi wote waliochaguliwa na serikali (TAMISEMI) kujiunga na Chuo cha Mipango wanahimizwa kuanza mapema maandalizi ya kujiunga na chuo.

Kwa wale ambao hawajachaguliwa na serikali wanaweza kufanya maombi moja kwa moja chuoni kwa njia ya mtandao kupitia mas.irdp.ac.tz

A. Kozi zitolewazo kwa ngazi ya Astashahada (Basic Technician Certificate)

- i. Astashahada ya Mipango ya Maendeleo Vijijini (Basic Technician Certificate in Rural Development Planning).
- ii. Astashahada ya Utawala na Usimamizi wa Maendeleo (Basic Technician Certificate in Development Administration and Management).
- iii. Astashahada ya Maendeleo ya Jamii (Basic Technician Certificate in Community Development).

B. Sifa za Mwombaji:

Mwombaji awe amehitimu KIDATO CHA NNE na kufaulu walau kwa kiwango cha alama “D” nne katika masomo yoyote isipokuwa masomo ya dini.

C. Muda wa Masomo:

Masomo ya Astashahada hutolewa kwa muda wa mwaka mmoja kwa mjumuisho wa mafunzo ya nadharia na vitendo.

D. Ada ya Masomo:

Ada kwa mwaka ni shilingi 925,000 ambayo hulipwa kwa awamu nne (kama ilivyochanganuliwa kwenye jedwali Na 1).

E. Kuripoti Chuoni

Kwa wanafunzi waliochaguliwa na serikali au wale watakao fanya maombi moja kwa moja chuoni wanapaswa kuripoti mwezi Septemba na kuwasili na vifuatavyo;

1. Vyeti vya masomo

Wanafunzi wanapaswa kuwasili na vyeti halisi (original certificates) vya kuzaliwa na vya taaluma (valid results slip au academic transcript)

2. Ada

Kwa wanafunzi wa kozi za Astashahada (Basic Technician Certificate, NTA Level 4) wakiwemo wale Waliochaguliwa na serikali ada yao ni Sh. 925,000/= inayolipwa kwa mchanganuo ufuatao;

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa ada kwa kozi za Astashahada (Certificate)

	SIKU YA KURIPOTI	BAADA YA MIEZI MIWILI	JUMLA
MUHULA WA KWANZA	Sh. 310,000	Sh. 200,000	Sh. 510,000
MUHULA WA PILI	Sh. 215,000	Sh. 200,000	Sh. 415,000
JUMLA KUU			Sh. 925,000

3. Mahitaji mengine nyingine

- Bima ya afya Sh. 50,400/= au Kadi ya bima ya afya ya NHIF inayofanya kazi
- Gharama ya vipimo vya afya Sh. 5000/= (vipimo vinafanyika kwenye zahanati ya chuo)
- Gharama ya hosteli Sh. 350,000/=

4. Malipo yote yatafanyika kwa **CONTROL NUMBER** zitakazotolewa kwenye mfumo wa usajili

5. Wanafunzi watajigharamia gharama za chakula, shajala (stationery) na mafunzo ya vitendo

6. Chuoni hakuna sare, ila wanafunzi wanapaswa kuvaa mavazi yanayokubalika kwa mujibu wa miongozo na taratibu za serikali.

Tunawakaribisha wote kujiunga na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini

F. Kwa msaada na maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi;

Kampasi kuu Dodoma: 0746 777 001, 0746 777 002 au 0746 777 006

Kituo cha Mafunzo Kanda ya Ziwa - Mwanza: 0748 000 648, 0748 002 460 au 0748 002 461

INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT & PLANNING

19 MAY 2022

P. O. BOX 138 - DODOMA.
SIGNATURE 

YAMETOLEWA NA:

OFISI YA MSAJILI WA WANAFUNZI
CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI
19/05/2022